# MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO ROBO YA KWANZA KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI-SEPTEMBA, 2021 KILICHOFANYIKA TAREHE 13.10.2021

**MAHUDHURIO YA WAJUMBE**

| NA. | JINA | CHEO |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. HUSSEIN I. SIMBA | MWENYEKITI |
| 2. | Ndg. JOHN K. MGALULA | KATIBU |
| 3. | Mhe. JONATHAN D HEMED | M/KITI H/W |
| 4. | Mhe. YAHAYA O. MASSARE | MJUMBE |
| 5. | Mhe. WILLIAM L. MASAKA | MJUMBE |
| 6. | Mhe. EMANUELY S. HAJU | MJUMBE |
| 7. | Mhe. MAGRETH S. MWALWAYO | MJUMBE |
| 8. | Mhe. REHEMA D. CHIZUMI | MJUMBE |
| 9. | Mhe. ELIZABETH E. KIDOLEZI | MJUMBE |
| 10. | Mhe. OBADIA L. MAZURI | MJUMBE |

**WAKUU WA IDARA NA VITENGO**

| NA. | JINA | CHEO |
|---|---|---|
| 1. | JOYCE J. MASOGA | KAIMU AFISA UTUMISHI (W) |
| 2. | DOREEN J. LUTAHANAMILWA | AFISA ELIMU MSINGI (W) |
| 3. | SEVERINE M. MZELOO | KAIMU AFISA UCHAGUZI (W) |
| 4. | FRED Y. LOTTI | MRATIBU UKIMWI (W) |
| 5. | MKINGUZI MGALULA | AFISA KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA (W) |
| 6. | NELIGWA MAIRA | MKAGUZI WA NDANI (W) |
| 7. | JONATHAN M. MUSHI | KAIMU AFISA TEHAMA (W) |
| 8. | KEVIN E. NGONYANI | AFISA ELIMU SEKONDARI (W) |
| 9. | NOHNY J. KIGODA | KAIMU AFISA USAFI NA MAZINGIRA (W) |
| 10. | JOHN B. CHAO | KAIMU AFISA MIFUGO NA UVUVI (W) |
| 11. | JOHN F. MAKOTTA | KAIMU AFISA ARDHI NA MALIASILI (W) |
| 12. | SUZANA J. MUSHI | AFISA MAENDELEO YA JAMII (W) |
| 13. | OMARI S. LIBUI | MTHIBITI UBORA ELIMU (W) |
| 14. | KURWA M. MBEYU | KAIMU MHANDISI WA UJENZI (W) |
| 15. | GILBERT M. KALANDA | KAIMU AFISA SHERIA (W) |
| 16. | GEOFREY KIBESA | KAIMU MWEKA HAZINA (W) |
| 17. | VALENCE KILASARA | MRATIBU WA TASAF (W) |
| 18. | ELIUTHA A. KIDENYA | AFISA TARAFA |
| 19. | GRACE MWAIGAGA | AFISA MIPANGO (W) |
| 20. | PATRICK N. KIGERE | AFISA MANUNUZI NA UGAVI (W) |

**SEKRETARIETI**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | CONSTANTINE MIHAMBO | MWANDISHI WA KIKAO |
| 2. | ADRIANA S. SIPPI | MWANDISHI WA KIKAO |

**AGENDA ZA KIKAO.**

1. KUFUNGUA KIKAO
2. KURIDHIA AGENDA
3. KUSOMA NA KUTHIBITISHA MIHTASARI YA VIKAO VYA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO VYA TAREHE 13.09.2021 NA TAREHE 24.09.2021.
4. YATOKANAYO NA KIKAO KILICHOPITA CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 13.09.2021.
5. TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWEZI SEPTEMBA, 2021.
6. TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA IDARA NA VITENGO MBALIMBALI KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA MWEZI JULAI-SEPTEMBA, 2021.
7. TAARIFA YA UKAGUZI WA NDANI ROBO YA KWANZA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.
8. TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA TSHS 250,000,000.00 KWA AJILI YA UPANUZI WA KITUO CHA AFYA MITUNDU.
9. TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA TSHS 34,421,030.23 KWA AJILI YA KAMPENI HARAKISHI YA CHANJO YA UVIKO-19.
10. MAOMBI YA KUONGEZEWA WIGO WA BAJETI WA FEDHA ZITOKANAZO NA TOZO ZA MIHAMALA KIASI CHA TSH 262,500,000.00 KWA AJILI YA UPANUZI WA KITUO CHA AFYA MITUNDU NA UMALIZIAJI WA BOMA LA DARASA SEKONDARI YA IDODYANDOLE.
11. MAOMBI YA KUONGEZEWA WIGO WA BAJETI WA FEDHA KUTOKA SERIKALI KUU NA WADAU WA EP4R, EGPAF NA GAVI KIASI CHA TSH 469,269,919.63 KWA AJILI YA KUTEKELEZA SHUGHULI ZA MAENDELEO.
12. MAOMBI YA KUONGEZEWA WIGO WA BAJETI WA FEDHA KIASI CHA TSH 3,610,000,000.00.
13. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA HOJA ZA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI (CAG) NA MKAGUZI WA NDANI.
14. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI-SEPTEMBA, 2021.
15. TAARIFA YA USAILI WA WAOMBAJI WA KAZI YA ULINZI NA UKUSANYAJI MAPATO KATIKA MAGETI.

16. TAARIFA YA MIRADI ILIYOTEMBELEWA NA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO TAREHE 11.10.2021.
17. MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI.
18. KUFUNGA KIKAO.

**MUHT/HW/ITG/FUM/VOL.II/NA.25/2021/2022: KUFUNGUA KIKAO**

Katibu aliwasalimu wajumbe na kuwaeleza kuwa kikao hiki ni kikao cha robo ya kwanza (Julai-Septemba), 2020/2021) baada ya maelezo hayo alimkaribisha mwenyekiti, Mwenyekiti aliwasalimu wajumbe na aliwaomba kuchangia vema agenda zilizopo mezani. Baada ya kusema hayo kikao kilifunguliwa saa 4:25 asubuhi.

**MUHT/HW/ITG/FUM/VOL.II/NA.26/2021/2022: KURIDHIA AGENDA**

Wajumbe waliridhia agenda na kushauri kikao kiendelee.

**MUHT/HW/ITG/FUM/VOL.II/NA.27/2021/2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MIHTASARI YA VIKAO VYA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO VYA TAREHE 13.09.2021 NA TAREHE 24.09.2021.**

Katibu aliwasilisha mihtasari ya vikao vya kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango vya tarehe 13.09.2021 na tarehe 24.09.2021, wajumbe walipokea mihtasari hiyo na baada ya kupitia ukurasa kwa ukurasa waliridhia isainiwe kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sahihi za kiofisi.

**MUHT/HW/ITG/FUM/VOL.II/NA.28/2021/2022: YATOKANAYO NA KIKAO KILICHOPITA CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 13.09.2021.**

Katibu aliwasilisha yatokanayo na kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 13.09.2021 baada ya kupitia utekelezaji hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

**MUHT/HW/ITG/FUM/VOL.II/NA.29/2021/2022: TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWEZI SEPTEMBA, 2021.**

Mweka Hazina Kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha taarifa ya mapato na matumizi ya mwezi Septemba, 2021 kama ifuatavyo:

**A: MAPATO**

Katika mwaka wa fedha **2021/2022** Halmashauri ya Wilaya ya Itigi imekadiria kukusanya na kutumia jumla ya Tshs 18,284,649,098.00 ikiwa ni ruzuku ya mishahara (P.E) Tshs 8,881,696,000.00, Ruzuku ya matumizi ya kawaida (O.C) Tshs 1,088,069,000.00 Ruzuku ya fedha za miradi ya maendeleo (Dev Grants) Tshs 6,410,893,265.00 na mapato ya ndani (Own Source) Tsh 1,903,990,833.00 kwa mchanganuo ufuatao;

JEDWALI 1: MAKADIRIO YA MAPATO NA MAPATO HALISI

| | CHANZO CHA MAPATO | MAKADIRIO 2021/2022 | MAPATO SEPTEMBA ,2021 | MAPATO JULAI-SEPTEMBA, 2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| MAPATO YA NDANI | Mapato Halisi | 1,735,560,000.00 | 231,915,705.75 | 501,239,485.55 | 29 |
| | Mapato Lindwa | 168,430,833.00 | 6,936,550.00 | 24,764,567.63 | 14 |
| | **Jumla Ndogo** | **1,903,990,833.00** | **238,852,255.75** | **526,004,053.18** | **27** |
| RUKUZU | Mishahara-Ruzuku | 8,881,696,000.00 | 701,801,060.00 | 2,089,731,120.00 | 23 |
| | Matumizi ya Kawaida (OC) | 1,088,069,000.00 | 89,345,749,99 | 198,488,746.00 | 18 |
| | Miradi ya Maendeleo | 7,149,117,265.00 | 357,108,335.00 | 445,232,945.00 | 6 |
| | **Jumla Ndogo** | **16,380,658,265.00** | **1,149,245,144.00** | **2,733,452,811.00** | **16** |
| **JUMLA** | **Jumla Kuu** | **18,284,649,098.00** | **1,384,520,850,00** | **3,259,496,864.00** | **17** |

JEDWALI 2: MAKADIRIO YA MATUMIZI NA MATUMIZI HALISI

| | CHANZO CHA MATUMIZI | MAKADIRIO 2021/2022 | MATUMIZI SEPTEMBA, 2021 | MATUMIZI JULAI-SEPTEMBA, 2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| MATUMIZI YA KAWAIDA | Mapato ya Ndani | 1,903,990,833.00 | 127,917,579.00 | 290,652,873.00 | 15 |
| | Ruzuku-OC | 1,088,069,000.00 | 52,902,703.00 | 115,949,917.00 | 10 |
| MATUMIZI YA MISHAHARA | Mapato ya Ndani | 17,860,863.00 | 990,000.00 | 2,970,000.00 | 16 |
| | Ruzuku ya Serikali | 8,881,696,000.00 | 701,801,060.00 | 2,089,731,120.00 | 23 |
| MIRADI YA MAENDELEO | Mapato Ndani | 738,224,000.00 | 0.00 | 0.00 | |
| | Ruzuku Fedha za Serikali Kuu | 2,583,057,000.00 | 4,045,000.00 | 107,200,000.00 | 4 |
| | Ruzuku-Fedha za Nje | 3,827,836,265.00 | 0.00 | 0.00 | |
| **JUMLA** | **Jumla Kuu** | **18,284,649,098.00** | **887,656,342.00** | **2,606,503,910.00** | **14** |

Baada ya kuipitia taarifa hii ukurasa kwa ukurasa mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe ili waweze kujadili taarifa ambapo Katibu wa kikao aliwashauri wajumbe kuhimiza wananchi kuchangia kwa kuwa mapato lindwa ni pamoja na ada na tozo mbalimbali za huduma, hivyo ni vema wananchi wakahamasishwa kuchangia huduma za Afya kwa kukata bima ya CHF iliyoboreshwaili kuongeza mapato.
Mwenyekiti wa kikao alieleza kuwa kwa kuwa uhamasishaji wa CHF iliyoboreshwa unakwenda kufanyika ni vema ambao watakata bima hizo wakatengewa dawa ili wanapoenda kutibiwa isilete changamoto ya ukosefu wa dawa. Alipongeza mapato kuwa yako vizuri na alisisitiza kusimamia vema mapato ya Halmashauri katika kipindi hiki cha mavuno ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kasma ambazo hazifanyi vizuri katika makusanyo katika kipindi hiki cha mavuno zinapaswa zikusanye.

**MUHT/HW/ITG/FUM/VOL.II/NA.30/2021/2022: TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA IDARA NA VITENGO MBALIMBALI KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA MWEZI JULAI-SEPTEMBA, 2021.**
Katibu aliwasilisha agenda na Mwenyekiti aliwakaribisha wawasilishaji ili wawasilishe taarifa zao;

- **IDARA YA FEDHA NA BIASHARA**

Taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Idara ya Fedha na Biashara kwa kipindi cha Mwezi Julai-Septemba, 2021 iliwasilishwa shughuli zilizofanyika ni kuandaa taarifa za mapato na matumizi za kila mwezi, kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri kwa vyanzo vyake vya ndani ambapo kwa kipindi cha mwezi Julai-Septemba, 2021 Halmashauri imekusanya Tshs 537,563,642.55 sawa na 28% ya lengo la mwaka Tshs 1,903,990,833.00, ufungaji wa hesabu za Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umekamilika na kuwasilishwa kwa vikao husika na kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Hoja za wakaguzi wan je na ndani ambazo zilijitokeza zimejibiwa kwa wakati, kusimamia upelekaji wa fedha katika ngazi za kutolea huduma za afya, elimu, vikundi na usimamizi wa usuluhishi wa kibenki kwa kila mwezi. Aidha, taarifa ilieleza changamoto ambazo Idara inakumbana nazo pamoja na mikakati ya utatauzi wa changamoto hizo. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kuipitia ukurasa kwa ukurasa hapakuwa na hoja iliyotokeza.

- **IDARA YA UTUMISHI NA UTAWALA**

Taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Idara ya Utumishi na Utawala kwa kipindi cha Julai-Septemba, 2021 iliwasilishwa shughuli zilizofanyika ni pamoja na mapokezi ya Watumishi wa tano (5) wamehamia na Watumishi kumi na moja (11) wamehama Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, Watumishi wawili (2) wamekoma Utumishi ambapo Mtumishi mmoja amefariki na Mtumishi mmoja amefukuzwa kazi. Wajumbe walipitia taarifa ukurasa kwa ukurasa na hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

- **IDARA YA UTUMISHI NA UTAWALA-SEHEMU YA USAFIRI**

Taarifa ya Utekelezaji wa kazi za Idara ya Utumishi na Utawala-Sehemu ya Usafiri kwa kipindi cha robo ya kwanza kuanzia mwezi Julai-Septemba, 2021 iliwasilishwa shughuli zilizofanyika ni pamoja na kuratibu na kupanga safari za magari, pikipiki na mitambo, kufuatilia na kusimamia matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo, kusimamia uendeshaji na uegeshaji wa magari, kutoa taarifa ya hali ya vyombo vya usafiri na mitambo ya Halmashauri. Aidha, taarifa ilieleza kuwa gari SM 3621 (TOYOTA LAND CRUISER D/CABIN). Wajumbe walipokea taarifa baada ya kupitia ukurasa kwa ukurasa walishauri ni vema gari ya TASAF ikafanyiwa matengenezo. Mkaguzi wa ndani Mkoa aliwashauri wajumbe na Wataalam kuomba vibali kwa ajili ya matengenezo ya magari mabovu kwa kuwa Halmashauri inatumia gharama kubwa kwenye utengenezaji wa magari TEMESA na bado hayatengemai. Katibu wa kikao alielelza kuwa gari ya TASAF itavutwa na matengenezo yatafanyika. Aidha, alitoa taarifa kuwa Halmashauri imepokea fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa Shule Shikizi Tshs 2,900,000,000.00, Shule za Sekondari Tshs 580,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 29 na Tshs 90,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Watumishi wa Idara ya Afya ambazo (3 in 1).
Alitoa taarifa kuwa Makamu Mwenyekiti ataingia katika Kamati za Kudumu kama mjumbe ikiwa ni pamoja na wajumbe ambao hawana Kamati za Kudumu wanapaswa kuwepo katika Kamati za kudumu angalau Kamati moja. Mwenyekiti wa kikao alipongeza kwa mapokezi ya fedha zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na alishauri pikipiki mbovu zitengenezwe au ziombewe kibali cha kuuza. Katibu alieleza kuwa magari mabovu yatakayouzwa ni yale ya SM tu, hivyo DFP na STL hazitauzwa kwa kuwa Halmashauri haina mamlaka ya kuuza magari hayo.

- **IDARA YA MIPANGO, TAKWIMU NA UFUATILIAJI**

Taarifa ya Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji kwa kipindi cha robo ya kwanza Mwezi Julai-Septemba, 2021 iliwasilishwa ambapo shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kuratibu maandalizi ya taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradiya maendeleo, kuandaa na kuwasilisha taarifa mbalimbali za utekelezaji, kuratibu maandalizi ya awali ya zoezi la Sensa ya watu na makazi, kuratibu uandaaji wanyaraka za kuombea fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kuhakikisha fedha zinazotolewabila kuwa na vifungu vya matumizi zinaombewa vifungu ili ziweze kutumika. Aidha, taarifa ilieleza changamoto ambazo Idara inakumbana nazo pamoja na mikakati ya utatauzi wa changamoto hizo. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kupitia ukurasa kwa ukurasa Mwenyekiti aliomba kupata ufafanuzi ni kwanini miradi mingine inasimamiwa na Wataalam wa Halmashauri Makao Makuu na miradi mingine inasimamiwa na ngazi za

chini? Afisa Mipango kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa kuna changamoto katika kutekeleza miradi iliyopo makao makuu, miradi iliyopo ngazi za chini inaenda vizuri licha ya kuwa inasimamiwa na Halmashauri. Alieleza kuwa changamoto ni Idara ya Ujenzi na Kitengo cha Manunuzi na Ugavi kutokushirikiana. Mganga Mkuu aliwaeleza wajumbe kuwa Vituo vya kutolea huduma vina mfumo hivyo vinaingiziwa fedha moja kwa moja kupitia akaunti za vituo ili ziweze kutekeleza miradi, Vijiji havina mfumo wa FFARS na ndio maana miradi hiyo inasimamiwa moja kwa moja Halmashauri. Katibu wa kikao alieleza kuwa mwongozo wa matumizi ya fedha haujatoka. Aidha, fedha zote zinapaswa kwenda kwenye Vituo ili kutekeleza miradi kwa kuwa vina mfumo wa FFARS na miradi inayokwenda kutekelezwa katika vijiji itasimamiwa na Halmashauri kwa kuwa akaunti zao hazijaunganishwa na mfumo wa FFARS.

- **KITENGO CHA MANUNUZI NA UGAVI**

Taarifa ya kitengo cha Manunuzi na Ugavi kwa kipindi cha robo ya kwanza kwa kipindi cha mwezi Julai-Septemba, 2021 ambapo Halmashauri imepanga kutumia Tshs 4,513,151,562.12 kwa ajili ya shughuli mbalimbali katika manunuzi. Aidha, kwa kipindi cha Julai-Septemba, 2021 Halmashauri imetumia jumla ya Tsh 108,614,794.66 sawa na 2% ya mpango wa manunuzi. Taarifa ilieleza changamoto pamoja na ufumbuzi wa changamoto hizo. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kuipitia ukurasa kwa ukurasa hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

- **KITENGO CHA UCHAGUZI**

Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Kitengo cha Uchaguzi katika kipindi cha robo ya kwanza Julai-Septemba, 2021 iliwasilishwa ambapo shughuli zilizofanyika ni pamoja na kuandaa taarifa ya fedha za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kwa ajili ya ukaguzi wa CAG, kutatua mgogoro wa uongozi kati ya Mwenyekiti wa Kijiji cha Itagata na Viongozi wa Chama cha Mapinduzi ngazi ya Tawi na Kata. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kuipitia ukurasa kwa ukurasa Mwenyekiti aliwashauri wajumbe kuwaelimisha viongozi waliopo katika maeneo yao wa vyama kufuata taratibu za kuwaondoa Wenyeviti wa Vijiji kwa kufuata utaratibu. Afisa sheria alishauri Waheshimiwa Madiwani pamoja na Viongozi wa Chama kuzisoma vema katiba za vyama kabla ya kutoa maamuzi. Mjumbe aliomba kupata ufafanuzi nini kifanyike katika maeneo ambayo yako wazi hayana Wenyeviti, Afisa Uchaguzi alieleza kuwa bajeti inaweza kuombwa kwa ajili ya kufanyika kwa uchaguzi mdogo.

- **KITENGO CHA SHERIA**

Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Kitengo cha Sheria kwa kipindi cha Mwezi Julai-Septemba, 2021 iliwasilishwa ambapo ilijumuisha shughuli mbalimbali ambazo zilitekelezwa ambazo ni kuishauri Halmashauri na wananchi masuala mbalimbali ya kisheria, kufanyia upekuzi mikataba mbalimbali, kusimamia kampuni ya Tumbaku iitwayo Magefa Growers Ltd ambayo haikuwa imelipa ushuru wa Zaidi ya Tshs 20,000,000/= uliotokana na mauzo ya Tumbaku kwa mwaka wa fedha 2020/21 ambapo mpaka sasa wamelipa kiasi chote kinachodaiwa Tsh 23,000,000/=. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kuipitia walishauri ni vema vyanzo vipya vya mapato ambavyo vimeshauriwa vikafanyiwa kazi ikiwa ni pamoja na kuanzisha maegesho ya malori katika kiwanja namba 1 kitalu x, Kata ya Mitundu iwekwe miundombinu ambayo itasaidia Halmashauri kupata mapato. Aidha, walishauri ni vema Afisa Sheria kwa kushirikiana na Afisa Kilimo wakasimamia wakulima wa Tumbaku wakalipwa fedha zao na Kampuni ya MAGEFA kabla ya msimu wa kilimo kuanza.

- **KITENGO CHA TEHAMA**

Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Kitengo cha TEHAMA kwa kipindi cha Mwezi Julai-Septemba, 2021 iliwasilishwa ambapo kitengo kimeendelea kusimamia mifumo mbalimbali inayopatikana kwenye miundombinu ya Ofisi ya Rais TAMISEMI pamoja na kimefunga na kuhakikisha mfumo wa ulipaji Serikalini unafanya kazi na wahusika wanatakiwa kuingia kwenye mfumo kulingana na mwongozo. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kuipitia ukurasa kwa ukurasa hapakuwa na hoja iliyojitokeza

**MUHT/HW/ITG/FUM/VOL.II/NA.31/2021/2022: TAARIFA YA UKAGUZI WA NDANI ROBO YA KWANZA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.**

Mkaguzi wa ndani aliwasilisha taarifa ya ukaguzi wa ndani robo ya kwanza kwa kipindi cha mwezi Julai-Septemba, 2021 ambapo Kitengo kilifanikiwa kutekeleza kazi mbalimbali ambazo ni ukaguzi wa usimamizi wa mapato na matumizi, kupitia majibu ya hoja za CAG, ukaguzi wa usimamizi wa mikataba, ukaguzi wa usimamizi fedha za EP4R, ukaguzi wa Mfuko wa pamoja wa Afya (HBF) na CHF, ukaguzi wa usimamizi wa mishahara, udhibiti wa ndani, ukaguzi wa mradi wa TASAF. Aidha taarifa ilieleza changamoto ya upungufu wa rasilimali (gari) za kutekeleza kazi za ukaguzi. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kuipitia ukurasa kwa ukurasa Mwenyekiti wa kikao aliagiza kuwa kila mwezi katika kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango hoja ambazo zimejitokeza zipunguzwe na taarifa iwasilishwe katika kikao.

**MUHT/HW/ITG/FUM/VOL.II/NA.32/2021/2022: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA TSHS 250,000,000.00 KWA AJILI YA UPANUZI WA KITUO CHA AFYA MITUNDU.**

Taarifa ya mapokezi ya fedha kiasi cha Tsh 250,000,000.00 kwa ajili ya upanuzi wa Kituo cha Afya Mitundu ambapo fedha hizi ni kwa ajili ya kujenga jengo la wagonjwa wa nje (OPD), kichomea taka (Incenerator) na maabara. Mganga Mkuu alieleza majengo yaliyopo katika Kituo cha Afya Mitundu ambayo ni jengo la

wagonjwa wan je (OPD), kichomea taka na jengo linalotumika kama wodi ya wanaume na wanawake. Kutokana na maelekezo yaliyoelekezwa kupitia barua iliyoleta fedha hizi alishauri majengo yanayohitajika ili kituo kiweze kufanya kazi yenye tija ni jengo la upasuaji (Operating Theatre), Jengo la mama na mtoto (Marternity Ward) na jengo la ufuaji (laundry). Wajumbe waliipokea taarifa baada ya kuipitia na kuijadili hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

**MUHT/HW/ITG/FUM/VOL.II/NA.33/2021/2022: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA TSHS 34,421,030.23 KWA AJILI YA KAMPENI HARAKISHI YA CHANJO YA UVIKO-19.**

Mganga Mkuu kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha taarifa ya mapokezi ya fedha kiasi cha Tsh 34,421,030.23 kwa ajili ya Kampeni harakishi ya chanjo ya UVIKO-19 toka Serikali Kuu ambapo fedha hizi zimekuja nje ya bajeti, wajumbe walipokea taarifa baada ya kupitia na kuijadili taarifa hii wajumbe waliridhia na walishauri Wataalam watoe elimu nzuri kuhusu chanjo zijazo.

**MUHT/HW/ITG/FUM/VOL.II/NA.34/2021/2022: MAOMBI YA KUONGEZEWA WIGO WA BAJETI WA FEDHA ZITOKANAZO NA TOZO ZA MIAMALA KIASI CHA TSH 262,500,000.00 KWA AJILI YA UPANUZI WA KITUO CHA AFYA MITUNDU NA UMALIZIAJI WA BOMA LA DARASA SEKONDARI YA IDODYANDOLE.**

Afisa Mipango kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha maombi ya kuongezewa wigo wa bajeti wa fedha zitokanazo na tozo za miamala kiasi cha Tshs 262,500,000.00 ambapo kiasi cha Tshs 250,000,000.00 ni kwa ajili ya upanuzi wa Kituo cha Afya Mitundu, fedha hizi zililetwa kwa ajili ya kujenga jengo la wagonjwa wa nje (OPD), kichomea taka (Incenerator) na Jengo la Maabara. Kutokana na uhitaji na ushauri wa kitaalam uliotolewa ilishauriwa kuwa yajengwe majengo matatu yaani jengo la upasuaji (Oparating Theatre), Jengo la mama na mtoto (Maternity Ward) na Jengo la ufuaji (Laundry). Wajumbe waliridhia fedha hizi zitumike kujenga majengo haya kama ilivyoshauriwa. Aidha, Tshs 12,500,000.00 kwa ajili ya umaliziaji wa boma la darasa Sekondari ya Idodyandole. Wajumbe walipokea taarifa na baada ya kupitia na kuijadili taarifa hii waliridhia maombi hayo na kushauri taratibu nyingine ziendelee.

**MUHT/HW/ITG/FUM/VOL.II/NA.35/2021/2022: MAOMBI YA KUONGEZEWA WIGO WA BAJETI WA FEDHA KUTOKA SERIKALI KUU NA WADAU WA EP4R, EGPAF NA GAVI KIASI CHA TSH 469,269,919.63 KWA AJILI YA KUTEKELEZA SHUGHULI ZA MAENDELEO.**

Afisa Mipango kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha maombi ya kuongezewa wigo wa bajeti wa fedha kutoka Serikali Kuu na wadau mbalimbali kiasi cha Tshs 469,269,919.63 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo ambapo Tshs 262,500,000.00 ni fedha za Serikali Kuu, Fedha za Wadau wa EP4R Tshs 155,417,139.55, GAVI Tshs 34,421,030.00 na EGPAF Tshs 16,931,750.08. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kupitia na kuijadili taarifa hii waliridhia maombi hayo na kushauri taratibu nyingine ziendelee.

**MUHT/HW/ITG/FUM/VOL.II/NA.36/2021/2022: MAOMBI YA KUONGEZEWA WIGO WA BAJETI WA FEDHA KIASI CHA TSH 3,610,000,000.00.**

Afisa Mipango kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha maombi ya kuongezewa wigo wa bajeti wa fedha Tsh 3,610,000,000.00 kwa ajili ya mgawo wa vyumba vya madarasa kwa Shule za Sekondari (vyumba vya madarasa 29 kila chumba Tshs 20,000,000.00 sawa na Tshs 580,000,000.00, mgao wa miundombinu ya vyumba vya madarasa vitakavyojengwa katika vituo 27 shikizi vya shule kwa vyumba 147 kila chumba Tshs 20,000,000.00 sawa na Tshs 2,940,000,000.00 na mgawo wa nyumba za Watumishi wa Afya 3 Tshs 90,000,000.00 . Wajumbe walipokea taarifa baada ya kupitia na kuijadili taarifa hii waliridhia maombi hayo na kushauri taratibu nyingine ziendelee.

**MUHT/HW/ITG/FUM/VOL.II/NA.37/2021/2022: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA HOJA ZA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI (CAG) NA MKAGUZI WA NDANI.**

Taarifa ya utekelezaji wa hoja za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali (CAG) ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Itigi ilipokea mapendekezo 89 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambayo yalitakiwa kufanyiwa kazi na Menejimenti hadi sasa mapendekezo 49 yamefanyiwa kazi na kubaki na mapendekezo 40 ambayo bado yanaendelea kufanyiwa kazi na Menejimenti. Katika Hoja za Mkaguzi wa Ndani, Menejimenti ilipokea mapendekezo 87 hadi tarehe 30, Juni, 2021 ambapo mapendekezo 15 yamefanyiwa kazi na kubaki mapendekezo 72 ambayo bado yanaendelea kufanyiwa kazi. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kuipitia ukurasa kwa ukurasa walishauri ni vema Hoja zikaendelea kujibiwa ikiwa ni pamoja na kutengeneza magari ambayo ni mabovu ili kuondoa hoja ya uwepo wa magari mabovu. Katibu alitoa taarifa kuwa gari mpya ambayo imenunuliwa imefika, aidha, gari nyingine itanunuliwa mwezi ujao. Wajumbe walipongeza Wataalam kwa jitihada wanazofanya katika kuhakikisha wanaleta maendeleo na kutatua changamoto zinazoikumba Halmashauri.

**MUHT/HW/ITG/FUM/VOL.II/NA.38/2021/2022: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI-SEPTEMBA, 2021.**

Afisa Mipango aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo robo ya kwanza kwa kipindi cha mwezi Julai-Septemba, 2021 ambapo Halmashauri ilipanga kutumia kiasi cha Tshs 7,149,117,265.00 katika kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo fedha toka Serikali kuu 2, 583,057,000.00, Mapato ya Ndani TShs 738,224,000.00 na Wadau Mbalimbali wa Maendeleo Tshs 3,827,836,265.00. Hadi kufikia tarehe 31, Septemba, 2021 fedha za miradi zilizopokelewa toka Serikali Kuu, Wadau wa Maendeleo na mapato ya ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni Tshs 548,776,435.84 sawa na asilimia 8 ya makisio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa miradi ni pamoja na kuchelewa kwa fedha za maendeleo kunakopelekea miradi kushindwa kukamilika kwa mwaka wa fedha husika, Halmashauri kukosa msamaha wa kodi katika utekelezaji wa miradi ya miradi ya maendeleo na hivyo kuongeza gharama ya utekelezaji. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kuipitia ukurasa kwa ukurasa Mwenyekiti wa kikao alishauri ni vema suala la manunuzi likasimamiwa vema katika miradi yote ambayo fedha imetolewa ili iweze kukamilika kwa wakati. Mjumbe aliomba ufanyike mgawanyo wa fedha za Serikali ambazo zimeletwa kwa ajili ya ujenzi wa Sekondari. Katibu wa kikao aliwaeleza wajumbe kuwa fedha hizi haziwezi kubadilishwa matumizi au kugawanywa, labda iwe imepelekwa mahali ambapo kuna hifadhi hivyo fedha hiyo itaombewa. Aidha, alisisitiza Waheshimiwa Madiwani kusimamia vema miradi ili hadi kufikia Disemba, 2021 inapaswa kuwa imekamilika.

**MUHT/HW/ITG/FUM/VOL.II/NA.39/2021/2022: TAARIFA YA USAILI WA WAOMBAJI WA KAZI YA ULINZI NA UKUSANYAJI MAPATO KATIKA MAGETI.**

Taarifa ya usaili wa waombaji kazi ya ulinzi na ukusanyaji mapato katika mageti iliwasilishwa ambapo jumla ya maombi arobaini na tatu (43) ya nafasi ya ukusanyaji wa mapato na nafasi kumi na sita (16) za kazi ya ulinzi wa mageti. Baada ya usaili kufanyika jumla ya waombaji thelathini na tano (35) kwa kazi ya ukusanya mapato walishinda usaili ambapo waombaji watano (5) hawakuhudhuria, mmoja aligushi cheti, mmoja anadaiwa na mwingine alionesha utomvu wa nidhamu wakatiwa usaili. Aidha, waombaji kumi na nne (14) walishinda katika usaili wa nafasi ya kazi ya ulinzi katika mageti ambapo muombaji mmoja hakuwasilisha cheti na muombaji mwingine mmoja hakuhudhuria. Hivyo orodha ya majina iliwasilishwa ili kamati itoe mapendekezo kama wahusika watafaa yawasilishwe katika Baraza la Madiwani ili kwa mamlaka waliyonayo iyajadili na kutoa maamuzi ili watakaokubaliwa waanze kukamilisha taratibu za kuleta wadhamini na kuanza kazi mwezi Novemba, 2021. Wajumbe walipokea taarifa na baada ya kuipitia na majadiliano ya kina waliridhia majina ya waombaji waliofuzu usaili kwa kupatiwa mikataba ya miezi mitatu (3) na kushauri taratibu nyingine ziendelee kama ilivyoelezwa.

**MUHT/HW/ITG/FUM/VOL.II/NA.40/2021/2022: TAARIFA YA MIRADI ILIYOTEMBELEWA NA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO TAREHE 11.10.2021.**

Afisa Mipango aliwasilisha taarifa ya miradi iliyotembelewa na Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango tarehe 11.11.2021 ambayo ni mradi wa ujenzi wa nyumba za watumishi, mradi wa ujenzi wa Zahanati katika Kijiji cha Mbugani, Mradi wa ujenzi Zahanati katika Kijiji cha Kamenyanga, miundombinu katika Shule ya Msingi Pentagoni, Ujenzi wa madarasa mawili na Ofisi katika Shule ya Msingi Mlowa na mradi wa ujenzi wa Zahanati katika Kijiji cha Kazikazi. Aidha, wajumbe wakati wa ziara hii walitoa ushauri katika miradi hii ili iweze kukamilika. Wajumbe walipokea taarifa hii baada ya kuipitia ukurasa kwa ukurasa Mwenyekiti aliagiza kuwa Zahanati ya Kazikazi iwe imekamilika hadi kufikia tarehe 31.10.2021.

**MUHT/HW/ITG/FUM/VOL.II/NA.41/2021/2022: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI.**

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kwa ajili ya mengineyo ambapo;

a) Viwekwe viti kwa ajili ya wananchi ambao watakua wakisubiri huduma katika ofisi za Wataalam wa Halmashauri.
b) Pongezi kwa ununuzi wa vifaa vya Ofisi ya Mwenyekiti wa Halmashauri.

Mwenyekiti alimkaribisha Mkaguzi wa ndani Mkoa ili aweze kuzungumza na wajumbe ambapo alieleza yafuatayo;

i. Kupitia kikao cha kamati ya fedha ufanyike ufuatiliaji wa hoja zilizoibuliwa, zilizojibiwa, zilizofutwa. Aidha, alieleza kuwa kwa sasa hoja za mkaguzi wa nje zipo 40 na hoja za mkaguzi wa ndani ni 72 hivyo mabadiliko yanatakiwa ili ziweze kupungua.
ii. Katika kila taarifa ya Idara na Vitengo ziwasilishwe hoja na namna zilivyoshughulikiwa katika kila kikao cha mwezi ili kuhakikisha hoja zinazobaki ni za ki-Sera.
iii. Maandalizi yafanyike mapema kuhusu miradi ya maendeleo inayokwenda kutekelezwa na namna ya kutumia fedha hizi na kuhakikisha miradi yote ni yenye kiwango kinachotakiwa.
iv. 40% ya makusanyo ya ndani ziende katika miradi kama ilivyoagizwa.
v. Waheshimiwa Madiwani wasimamie miradi iliyopo katika Kata zao.
vi. Manunuzi ya vifaa vya ujenzi yafanyike kwa ujumla ili kupunguza gharama.

**MUHT/HW/ITG/FUM/VOL.II/NA.42/2021/2022: KUFUNGA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili aweze kuahirisha kikao, Mwenyekiti alimshukuru Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri kwa kuridhia waheshimiwa Madiwani kuwepo katika Kamati angalau moja ya kudumu ya Halmashauri. Aliagiza Afisa Manunuzi na Ugavi kufanya kazi kwa bidii na kwa wakati ili miradi iweze kukamilika kwa wakati. Alisisitiza Wataalam kushughulikia changamoto zinazojitokeza ikiwa ni pamoja na kutekeleza maagizo ya kamati hii. Alisisitiza kushughulikia dokezo la vitendea kazi vya ofisi ya Mwandishi wa Vikao. Kupunguza madeni ya watumishi na Wananchi (Wazabuni) wanaoidai Halmashauri. Baada ya hapo aliahirisha kikao saa 7:23 mchana.

**UMETHIBITISHWA NA KUSAINIWA NA,**

..........................
John K. Mgalula
**Katibu**
Tarehe **11.11.2021**

..........................
Hussein I. Simba
**Mwenyekiti**
Tarehe **11.11.2021**